



Ushauri kwa Wazazi kuwalinda Watoto Mtandaoni.

Mzazi au Mlezi ndiye mwalimu namba moja wa mtoto wake na kwa kiasi kikubwa sana mtoto hujifunza na kuiga mambo mbalimbali kutoka kwa mzazi au mlezi wake.

Endapo Mzazi au Mlezi ataruhusu mtoto wake kutumia mitandao kupitia vifaa vya kieletroniki kama kompyuta, tableti au simu ya mkononi basi ana jukumu la kumlinda na kuhakikisha usalama wake.



Ewe Mzazi au Mlezi zingatia yafuatayo;

1. Muhamasishe Mtoto kutumia mitandao ili umsaidie kwenye masomo yake (kitaaluma Zaidi) na si vinginevyo.
2. Jifunze kila kitu kwa mapana kuhusu mtandao. Kuzoea mtandao hakutakusaidia tu kuelewa athari, lakini pia kukusaidia kuzungumza na watoto wako.
3. Weka mipaka ya mambo ambayo mtoto wako anaweza na ambayo hawezi kuyafanya mtandaoni. Ni muhimu kuweka masharti kwa mtoto wako ili ajue wajibu wake na mipaka yake pindi awapo mtandaoni. Usisubiri hadi kitu kibaya kitokee kwake.
4. Weka udhibiti ikiwa ni pamoja na kuchuja maudhui yasiyofaa kwa kutumia programu maalumu za kompyuta (parental control programs) kwenye vifaa vyako vya kompyuta.
5. Mfundishe mtoto wako namna ya kulinda taarifa binafsi. Kwa kawaida siyo salama kuchapisha taarifa binafsi mtandaoni kama nambari za simu, anwani, nywila (password) na namba ya kadi ya benki. Ikiwa wahalifu wanapata taarifa hizi, wanaweza kuzitumia vibaya dhidi yake au familia yako.
6. Zungumza na mtoto wako juu ya matumizi sahihi na salama ya mtandao ikiwemo mitandao ya kijamii ambayo huruhusu watumiaji wake kushiriki picha, video na majadiliano kati ya marafiki au wageni.
7. Muhamasishe mtoto wako kutoa taarifa kwako endapo atakutana na tatizo lolote mtandaoni. Ikiwa mtoto wako anapata tatizo mtandaoni, mshauri aje kwako au awasiliane nasi kupitia tovuti yetu au namba za simu badala ya kuacha. Kumbuka kwamba upo uwezekano wa mtoto wako kukumbana na maudhui yasiyofaa au tukio hatarishi mtandaoni, hata kama wanafanya kila kitu kwa usahihi.

**Kwa taarifa
na msaada
zaidi
Wasiliana
nasi kupitia**



TANZANIA COMPUTER EMERGENCY RESPONSE TEAM (TZ-CERT)

Mawasiliano Towers
20 Sam Nujoma Road
P.O. Box 474
14414, Dar Es Salaam.
TANZANIA

Tel: +255 22 2412011-2
+255 22 2199760-8
Mob: +255 784 558270-1
Fax: +255 22 2412 038
Email: cop@tzcert.go.tz
Website: <https://www.tzcert.go.tz>

PGP Key ID: EF916FCAEED630F6

PGP Key Fingerprint: 0A1C CF48 D623 9BE7 676B 4C03 EF91 6FCA EED6 30F6

